

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE
MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA,
UONGOZI NA MIPANGO KILICHOKETI TAREHE 12/11/2021
KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI.

KUMB NA.03/FUM/2021/2022/27– MAHUDHURIO.

WAJUMBE WALIOHUDHURIA:-

- | | | |
|----------------------------------|---|-------------------|
| 1. Mh. Diwani Yusuph Mohamed | - | Mwenyekiti |
| 2. Mh. Diwani Leokadia Kasase | - | Makamu Mwenyekiti |
| 3. Mh. Diwani Rahel Sololo | - | Mjumbe |
| 4. Mh. Diwani Lameck Warangi | - | Mjumbe |
| 5. Mh. Diwani Mary S.Nchiba | - | Mjumbe |
| 6. Mh. Diwani Juma C.Lushiku | - | Mjumbe |
| 7. Mh. Diwani Boniphace Shitobel | - | Mjumbe |
| 8. Mh. Diwani Amos Herman | - | Mjumbe |

WATAALAM WALIOHUDHURIA:-

- | | | |
|--------------------------|---|-------------------------------------------|
| 1. Lutengano G. Mwalwiba | - | Mkurugenzi Mtendaji (W) - Katibu |
| 2. Majaga Tandasi | - | Kaimu Afisa Utumishi (W) |
| 3. Stanley Kabelinde | - | Kaimu Mweka Hazina (W) |
| 4. Sylvia Rwehabura | - | Afisa Mipango (W) |
| 5. Rashid S.Omary | - | Kny, Afisa Mifugo na Uvuvi(W) |
| 6. Michael Serakikya | - | Kaimu Afisa Maliasili (W) |
| 7. Dominico A .Shilingo | - | Mhandisi Ujenzi (W) |
| 8. Francis I. Kailembo | - | Kaimu Afisa Mazingira (W) |
| 9. Shadraka Kabanga | - | Afisa Elimu Msingi (W) |
| 10. Suleiman D. Kuhanga | - | Mthibiti ubora wa Elimu (W) |
| 11. Zachariah P. Isaac | - | Kny, Mganga Mkuu (W) |
| 12. Joseph S. Machibya | - | Afisa kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W) |
| 13. Philbert Nyangahondi | - | Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 14. Sadi Kambi | - | Afisa TEHAMA |
| 15. Sungura M. F | - | Katibu TSC |
| 16. Obeid Moshi | - | Mkaguzi wa ndani |
| 17. Ladislaus W. Magaso | - | Afisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 18. Joseph N. Komba | - | Mwanasheria wa Halmashauri |
| 19. Atupakisye Martin | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha habari (W) |
| 20. Tumbo Madaraka | - | Afisa Tarafa Ushirombo |
| 21. Dafosa Shayo | - | Afisa Nyuki (W) |
| 22. Mashaka C. Amani | - | Kaimu Afisa Tarafa Ushirombo. |
| 23. Lameck Mlugwa | - | Afisa Tarafa Siloka |
| 24. Mayunga M. Masunga | - | Afisa Tarafa Bukombe |
| 25. Mwita S. J. | - | Mkuu wa Kitengo cha manunuzi (W) |
| 26. Agustino Simbeye | - | Kny, Afisa Ardhi (W) |
| 27. Grevas N. Nkononziku | - | Kaimu Afisa Uchaguzi (W) |
| 28. Idrisa B. Kheri | - | Mwandishi wa vikao |
| 29. Joshua Makenza | - | Sekretarieti |
| 30. Petro Lugwisha | - | Mwandishi wa Vikao |

KUMB NA.03/FUM/2021/2022/28-WAKARIBISHWA

Hakuna.

KUMB NA.03/FUM/2021/2022/29 – WAJUMBE WASIOHUDHURIA:

1. Mh. Dotto Biteko (Mb) - Kwa taarifa

WATAALAM WASIOHUDHURIA:

1. Hakuna.

KUMB NA.03/FUM/2021/2022/30 – KUFUNGUA KIKAO.

Katibu kabla ya kumkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao alimshukuru Mwenyeki Mungu kwa kuwajalia wajumbe uzima na afya njema. Baada ya hapo Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao. Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 4.40 asubuhi.

KUMB NA.03/FUM/2021/2022/31 – KURIDHIA AGENDA.

Katibu wa kikao alisoma agenda za kikao na kupokelewa na wajumbe. Baada ya hapo wajumbe waliridhia agenda zote kama zilivyowasilishwa.

KUMB NA.03/FUM/2021/2022/32 – KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 26/10/2021.

Muhtasari husika ulisomwa mbele ya kikao na kupokelewa na wajumbe. Baada ya hapo Muhtasari ulitiwa saini na Mwenyekiti na Katibu kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao cha tarehe 26/10/2021.

KUMB NA.03/FUM/2021/2022/33 – YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 26/10/2021.

Taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya kikao cha tarehe 26/10/2021 iliwasilishwa mbele ya kikao na kupokelewa na wajumbe na kujadiliwa.

Hoja ya Kwanza ilikuwa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) iendelee kufuatilia wamiliki wa vitalu vya uchimbaji wa madini ya dhahabu katika mgodi wa Msitu wa Hifadhi ya Halmashauri ya Wilaya ili walipe ushuru wa Halmashauri na kufunga mkataba. Kikao kilifahamishwa kuwa jumla ya shilingi 6,020,000/= zimelipwa na wamiliki wanne kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama ifuatavyo; Umoja Gold Mining amelipa shilingi 1,505, 000/=, Saul & Partners amelipa shilingi 1,505,000/=, Gold Miti & Partners amelipa shilingi 505, 000/=,. Hatua inayofuata ni kufunga mikataba ya uchimbaji wa madini.

Baada ya maelezo hayo Mh. Boniphace Shitobelo alitaka kujuu kwa nini baadhi ya wamiliki wa vitalu kati yao hawajalipia vitalu vyao. Mkurugenzi Mtendaji (W) alijibu hoja hiyo kuwa baadhi ya wamiliki wa vitalu wameahidi kulipia vitalu vyao mwezi Desemba, 2021.

Hoja iliyofuata ilikuwa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kufanya tathmini kwenye vyanzo vya mapato ya ndani ambapo kikao kilifahamishwa kwamba tathmini ya vyanzo vya mapato ya ndani itafanyika kabla ya kikao cha mwezi Oktoba, 2021. Wajumbe walikubaliana na maelezo hayo na kusitiza azimio hili lipewe kipaumbele.

Hoja nyingine ilikuwa Mkurugenzi Mtendaji (W) aendelee kuwasiliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupata ushauri juu ya ulipaji wa fidia ya ardhi ilipojengwa shule ya Sekondari Nyasato iliyoko Wilaya ya Mbogwe. Kikao kilifahamishwa kwamba Mkurugenzi Mtendaji (W) amemtuma Afisa Utumishi kufuatilia majibu ya barua iliyotumwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakapokuwa Dodoma kikazi.

Baada ya hapo kikao kilipokea taarifa ya madeni ya wakusanyaji wa mapato ya Halmashauri (Defauters). Katika kuchangia hoja Mh. Lameck Warangi na Mh. Juma C. Lushiku kwa nyakati tofauti walihoji ni kwa nini fedha nyingi kiasi hicho hazijapelekwa benki.

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwaeleza wajumbe kuwa kuna madeni yanayotokana na mfumo na mengine ni ya wakusanyaji wa mapato. Lakini kuna changamoto zake kwani wapo waliopewa namba ya malipo kwa ajili ya kulipia huduma kwenye Halmashauri lakini hawakulipa. Kwa upande wa Issa Msole POS yake ina matatizo ambayo yanafanyiwa kazi TAMISEMI. Hata hivyo Mkurugenzi Mtendaji (W) aliahidi kuyapunguza madeni hayo walau yafikie asilimia 35% ya makusanyo ya mwezi.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri alikieleza kikao kuwa Charles John, Frednand Masembo, Simoni Hakili John na Issa Msole ni wadaiwa sugu, alipendekeza wanyang'anywe POS. Aidha, Mh. Juma C. Lushiku alieleza kuwa kuna wakusanyaji wa mapato wanaodaiwa fedha nyingi lakini wao wanasema hawadaiwi kiasi hicho. Alipendekeza watumishi wanaodaiwa wasipewe POS kwa sababu baadhi ya watumishi ndio wanaongoza kwa kupoteza mapato. Aliendelea kueleza kuwa kuna chanzo cha mapato kimekusanya fedha bila POS kuanzia tarehe 1/11/2021 mpaka tarehe 11/11/2021 na pia kuna siku soko kuu la Ushirombo halikuwa na wakusanyaji wa ushuru. Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwaeleza wajumbe kuwa hatuwezi kufuta deni la mtu pasipokufanya uchunguzi. Wajumbe walijadili hoja hiyo kwa muda mrefu na hatimaye kikao kilazimia kuwa; -

Azimio

- Watumishi wanaokusanya mapato ya Halmashauri ambao hawajapeleka fedha benki wachukuliwe hatua kali za kisheria na watumishi wafunge mikataba.

Hoja iliyofuata ilikuwa inahusu kutoa semina kwa Waheshimiwa Madiwani juu ya matumizi ya mifumo ya utunzaji wa hesabu za fedha za Halmashauri ambapo kikao kilifahamishwa kuwa semina itafanyika mwezi Januari 2022 kwa kutumia wataalam wa Halmashauri. Wajumbe walikubaliana na maelezo hayo. Hata hivyo Waheshimiwa Madiwani walieleza kuwa tangu walipoapishwa hawajapata semina ya kuwajengea uelewa juu ya uendeshaji wa majukumu yao ya kila siku. Kwa hali hiyo waliomba waitwe wataalam kutoka chuo cha Serikali za mitaa cha Hombolo (LGTI) kutoa semina kwa Madiwani. Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwaeleza Waheshimiwa Madiwani kuwa suala la mifumo linabadilika kila siku hata Wakurugenzi waliomba mafunzo kama hayo tangu mwaka jana lakin wamepewa mafunzo Mkoani Geita kwa siku mbili tu. Baada ya maelezo hayo kikao kiliazimia kuwa;

Azimio

- Wataalam kutoka chuo cha Serikali za mitaa cha Hombolo waitwe kuja kutoa semina ya uelewa wa majukumu ya Madiwani.

Suala lingine lilifuata lilikuwa kamati ya mapato ilete kwenye kikao mapendekezo ya vyanzo vya mapato vitakavyokusanya na mawakala na vile vitakavyobaki kwa watumishi. Kikao kilifahamishwa kuwa Menejimenti inapendekeza chanzo cha ushuru wa madini ya ujenzi kikusanywe na mawakala na vyanzo vingine vitaendelea kukusanya na watumishi. Katika kuchangia hoja Mh. Lameck Warangi alitoa malinganisho ya mapato ya miaka mitatu katika ushuru wa Ng'ombe mnadani kuwa mapato wakati wa mawakala yalikuwa makubwa kuliko kipindi hiki cha watumishi. Alieleza kuwa watumishi wanachelewa kwenda mnadani na kusababisha mapato mengine kutoroshwa. Alipendekeza vyanzo vingine kama vile ushuru wa maegesho ubinafsishwe. Mh. Juma C. Lushiku alipendekeza Menejimenti ichague vyanzo vingine vitano vikusanywe na mawakala ili kufanya malinganisho. Kwa upande wake Mh. Boniphace Shitobelo aliunga mkono hoja na kueleza kuwa watendaji wameshindwa kukusanya mapato ipasavyo. Alipendekeza Menejimenti isimamie ukusanyaji wa mapato yanayovuja na pia minada ya Ng'ombe na maegesho yote wapewe mawakala pamoja na maegesho na vyanzo vyote vikubwa.

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwaeleza wajumbe kuwa Serikali haitaki mawakala na hili siyo la Bukombe tu bali ni Nchi nzima. Alishauri Waheshimiwa Madiwani kutoa taarifa mahali ambapo wanaona mapato yanapotea ili waboreshe.

KU MB. NA. 03/FUM/2021/2022/34 – TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KUISHIA 30/09/2021.

Taarifa iliwasilishwa mbele ya kikao na kupokelewa na wajumbe. Taarifa hiyo ilibainisha kuwa hadi kufikia tarehe 30/09/2021 Halmashauri ilikusanya jumla ya Tsh. 453,252,304.24 ikiwa ni sawa na 16.84% ya makisio ya mapato ya ndani kwa mwaka na Tsh. 6,695,879,474.41 sawa na 19.35% ya makisio ya mapato yote kwa mwaka. Pia Halmashauri kwa kipindi cha kuishia tarehe 30/09/2021 ilitumia jumla ya Tsh. 15,974,945,805.00 ikiwa ni sawa na asilimia 17.23%. Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili ukurasa kwa ukurasa.

Katika kuchangia hoja Mh. Juma C. Lushiku alitaka kujua ni kitu gani kimesababisha kubadilisha wakusanyaji wa mapato kwenye ushuru wa stendi na maegesho Ushirombo na Uyovu. Aliendelea kueleza kuwa kutokana na mabadiliko hayo mapato hayakukusanya kwa muda wa siku saba. Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwaeleza wajumbe kuwa mabadiliko yanafanya na Mkurugenzi Mtendaji (W) na siyo kweli kwamba mapato hayakukusanya kwa muda wa siku saba. Mabadiliko hayo yamefanyika kwa lengo la kuboresha ukusanyaji wa mapato na hadi sasa mapato yameongezeka.

Baada ya hapo wajumbe walitaka kujua kwa nini kifungu cha Utawala Madiwani kimetumia shilling 31,155,700.00 wakati Madiwani bado hawajalipwa posho zao za miezi mitatu. Kaimu Mweka Hazina (W) aliomba hoja hiyo aichukue ili aweze kufuutilia na kutoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Halmashauri. Wajumbe waliafiki.

KUMB NA.03/FUM/2021/2022/35 – TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA IMF KATIKA MIRADI YA AFYA NA ELIMU ZILIZOKO NJE YA BAJETI 2021/2022.

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha mapokezi ya fedha za uviko – 19 (IMF) kiasi cha Tsh. 2,530,000,000 katika utekelezaji wa miradi ifuatayo;

- Ujenzi wa madarasa Elimu Sekondari. Tsh 1,280,000,000
- Ujenzi wa madarasa Elimu Msingi Tsh. 860,000,000
- Ujenzi wa jengo la dharura Hospitali wa Wilaya Tsh. 300,000,000
- Ujenzi wa nyumba ya watumishi three in one Tsh. 90,000,000

Pia Mkurugenzi Mtendaji (W) ameomba majengo hayo yajengwe kwa njia ya Force Account kwa kuzingatia taratibu na mwongozo uliotolewa. Baada ya taarifa hiyo waheshimiwa Madiwani walialiki, wakaelekeza Fedha zote za uviko ujenzi utumie njia ya "Force Account" pia baadhi ya vifaa vinunuliwe kwa pamoja viwandani kwa mawakala.

KUMB NA.03/FUM/2021/2022/36 – TAARIFA YA MKAGUZI WA NDANI ROBO YA KWANZA 2021/2022.

Taarifa ilijwasilishwa mbele ya kikao na kupokelewa na wajumbe. Taarifa hiyo ilibainisha kuwa hadi kufikia tarehe 30/09/2021 utekelezaji wa hoja ilikuwa kama ifuatavyo;

- Hoja za nyuma kwa mwaka 2017/2018 zilikuwa 135 zimejibiwa hoja 130 bado hoja 5,
- Mwaka 2018/19 zilikuwa hoja 196 zimejibiwa na kufungwa hoja 188 bado hoja 8,
- Mwaka 2019/2020 zilikuwa hoja 89 zimejibiwa 57 bado hoja 32,

Wajumbe walipitia hoja zote na kisha walisisitiza hoja zote zijiwi na kufungwa.

KUMB NA.03/FUM/2021/2022/37 – TAARIFA YA KITENGO CHA SHERIA ROBO YA KWANZA 2021/2022.

Taarifa ilivasilishwa mbele ya kikao na kupokelewa na wajumbe. Taarifa hiyo ilhusisha kesi ya Ardhi Na. 81/2020 ya ndugu Salum Mohamed na wenzake kumi na tatu dhidi ya Afisa ardhi wa Wilaya ya Bukombe na kesi ya madai Na.03/2019 ya ndugu Phinias Kalokola dhidi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi Mtendaji (W) ya Bukombe. Wajumbe walipitisha mashauri hayo yaendelee kusikilizwa.

KUMB NA.03/FUM/2020/2021/38 – TAARIFA YA BODI YA MANUNUZI ROBO YA KWANZA 2021/2022.

Katibu wa kikao alitoa taarifa kuwa hadi kufikia tarehe 30/09/2021 manunuizi yaliyofanyika yalikuwa jumla ya shilingi 44,572,349 ambayo yalihusisha ununuizi wa vifaa na huduma za kitaalam.

Wajumbe walipitisha taarifa hiyo kama ilivyowasilishwa.

KUMB NA.03/FUM/2021/2022/39 – TAARIFA YA UTAWALA ROBO YA KWANZA 2021/2022.

Kaimu Afisa Utumishi (W) aliwasilisha taarifa ya Utawala mbele ya kikao na kupokelewa na wajumbe.

Taarifa hiyo ilibainisha mambo yafuatayo:-

1. Idadi ya watumishi

Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe hadi kufikia Septemba, 2021 ilikuwa na jumla ya watumishi 2,176 kati ya watumishi 2,615 wanaohitajika, hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 439 kwa mujibu wa Ikama.

2. Maeneo ya Utawala

Hadi kufikia mwezi Septemba, 2021 maeneo ya Utawala yalikuwa kama yalivytangazwa katika notisi ya mgawanyo wa maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Mji) na amri ya mgawanyo wa maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) mwaka 2019.

3. Taarifa mbalimbali.

Taarifa zilizowasilishwa ni;

• Taarifa kuhusu vifo vya watumishi,

Kikao kilipokea taarifa ya kifo cha mtumishi ndugu Joseph M. Msusa (WEO) aliyeefariki tarehe 27/07/2021.

4. Taarifa kuhusu watumishi waliohama/kuhamia.

Kikao kilipokea taarifa kuwa watumishi wafuatao wamehama na kuhamia Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe.

1. Dionis M. Myinga (Mkurugenzi) kutoka Bukombe DC kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Hai,
2. Lutengano G. Mwalwiba (Mkurugenzi) kibali cha Katibu Mkuu TAMISEMI kutoka Magu DC kwenda Bukombe DC,
3. Majaga Tandas (Afisa Utumishi) kibali cha Katibu Mkuu TAMISEMI kutoka Ifakara TC kwenda Bukombe DC,
4. Leah G. Kibaki (Afisa Utumishi) kibali cha Katibu Mkuu TAMISEMI kutoka Bukombe DC kwenda Manispaa ya Nzega,
5. Pendo ndalahwa (Mwalimu) kibali cha Katibu Mkuu TAMISEMI kutoka Tunduru DC kwenda Bukombe DC,
6. Justina Komugisha Josephat (Mwalimu) kibali cha Katibu Mkuu TAMISEMI kutoka Kibiti DC kwenda Bukombe DC,
7. Neema E. Sanga (Mwalimu) kibali cha Katibu Mkuu TAMISEMI kutoka Busokelo DC kwenda Bukombe DC
8. Gloria Cunbert (Mwalimu) kibali cha Katibu Mkuu TAMISEMI kutoka Nyang'hwale DC kwenda Bukombe DC.

Taarifa ya mapokezi ya gari jipy SM 14038.

Kikao kilipokea taarifa ya mapokezi ya gari jipy SM 14038 aina ya double cabin.

Taarifa ya ukaguzi wa miradi.

Taarifa ilitolewa kuwa kamati ya Fedha,Uongozi na Mipango ilifanya ukaguzi huo tarehe 10/11/2021 na trehe 11/11/2021 katika maeneo yafuatayo;

1. Ukarabati wa machinjio ya wanyama Katente,
2. Ukarabati wa vyoo vya soko kuu la Ushirombo,
3. Ujenzi wa kituo cha afya Bufanka,
4. Kuona kiwanda cha kufyatua matofali ya block cha Halmashauri ya wilaya ya Bukombe
5. Ujenzi wa shule ya Sekondari Ng'anzo,
6. Ujenzi wa miundombinu ya majengo katika kituo cha afya Namonge,
7. Ujenzi wa maghala ya kuhifadhi nafaka kwa ajili ya kuzuia sumu kuvu,
8. Ujenzi wa stendi ya mabasi Runzewe na ujenzi wa choo cha soko la Lyobahika. Kamati ilishauri kasi ya ujenzi wa miradi hiyo iongezeke ili miradi ikamilike kwa wakati na pia kuwepo na usimamizi wa karibu ili miradi hiyo iendane na thamani ya fedha.

KUMB NA.03/FUM/2021/2022/40 – MAAGIZO YA SERIKALI.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alitoa taarifa kuwa TASAF imekuja kwa utaratibu mwingine wa miradi taarifa italetwa kwenye vikao.

KUMB NA.03/FUM/2021/2022/41 – KUFUNGA KIKAO.

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufunga kikao baada ya dondo zote kujadiliwa na kumalizika.

Mwenyekiti kabla ya kufunga kikao aliwashukuru wajumbe kwa michango yao ya mawazo.Baada ya hapo Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 9.11 Alasiri kwa kusisitiza utekelezaji wa maazimio ya kikao.

"UMETHIBITISHWA"

MWENYEKITI

JINA YUSUPH MOHAMMED
SAINI Yusohamed.
TAREHE 17/12/2021

KATIBU

JINA LUTENGANO GM
SAINI G. Dejan
TAREHE 17/12/21